

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3

Baruapepe: cg@dcea.go.tz

Tovuti: www.dcea.go.tz

Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni,
S.L.P. 80327,
Dar es Salaam.

TAARIFA KWA UMMA

MAHAKAMA YAWAHUKUMU KIFUNGO CHA MAISHA ABDUL NSEMBO NA MKEWE

Dar es Salaam, 01 Aprili, 2021:

Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imewahukumu kutumikia kifungo cha maisha jela washtakiwa Abdul Issa Nsembo (47) na mkewe Shamim Omari Mwasha (43) kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevy aina ya Heroin hydrochloride zenyet ukiti wa gramu 275.40.

Hukumu hiyo imetolewa tarehe 31 Machi 2021 mbele ya Jaji Elinaza Luvanda wa Mahakama hiyo baada ya ushahidi uliotolewa Mahakamani hapo kuthibitisha pasipo shaka yoyote kwamba, washtakiwa wanajihuisha na biashara ya dawa za kulevy.

Sambamba na hukumu hiyo, Mahakama imetoe amri ya kutaifishwa kwa gari aina ya Land Rover Discovery yenye namba za usajili T.817 BQN kwa kuwa lililotumika kwenye uhalifu huo; pamoja na kuteketezwa kwa dawa walizokamatwa nazo. Hata hivyo, washtakiwa wameonesha kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa hivyo wamekusudia kukata rufaa.

Katika shauri hilo, upande wa Jamhuri uliongozwa na wakili wa Serikali Costantine Kakula na Veronica Matikila wakili mwandamizi wa Serikali, huku upande wa utetezi ukiongozwa na mawakili wa kujitegemea, ambao ni Juma Nassoro akimtetea Nsembo na Hajra Mungura akimtetea Shamim.

Washtakiwa wametiwa hatiani kwa kukiuka Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy Namba 5 ya Mwaka 2015 kama ilivyorejewa Mwaka 2019.

Nsembo na mkewe, walikamatwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta tarehe 1 Mei, 2019 katika eneo la Mbezi Beach ‘A’ Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni Jijini Dar es salaam, wakiwa na kiasi hicho cha dawa za kulevyta na kufunguliwa shauri la uhujumu uchumi namba 4 ya mwaka 2020.

Imetolewa na,



Frolence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta

